# TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**Salamu za Faraja kwa Wahanga wa Mafuriko Hanang, 06/12/2023**

Kanisa la Tanzania Assemblies of God kwa pamoja na kwa umoja wetu tunaungana na ndugu zetu wa Hanang kuomboleza vifo vya wapendwa wetu 63 vilivyosababishwa na janga zito na la kustusha la mafuriko na matope *(mudslide)*. Tunawapa pole sana, kwa janga hili ambalo limetuumiza na kutuhuzunisha sana mioyo yetu sisi sote.

Mafuriko haya yaliyosababishwa na mvua nyingi usiku wa kuamkia Disemba 3, 2023, yamewaathiri watu zaidi ya 21,000 katika maeneo ya Hanang, Katesh na Gendabi, wengi wao wakiwa wanawake na watoto; na kuharibu hekari nyingi za mazao, nyumba na mali mbali mbali.

Katika janga hili, kanisa letu la TAG limepoteza washirika zaidi ya 13 waliofariki, jengo moja la kanisa letu limechukuliwa lote na mali nyingi zingine zimepotea kabisa. Kiwango cha hasara na uharibifu ni mkubwa mno na watu wako katika hali ya uhitaji wa kiroho na wana-mahitaji mbalimbali ya kibinadamu.

Aidha tunaishukuru kwa dhati Serikali yetu, kwa kufika kwa haraka, na viongozi wakubwa mbalimbali kutembelea maeneo hayo ya tukio na kutuma zaidi ya waokoaji 400 ikiwepo timu ya wataalam na madaktari, ambao wameendelea kufanya kazi usiku na mchana pasipo kujali hali mbaya ya hewa, matope, na baridi kali ili kuhakikisha huduma za mahitaji ya muhimu ya watu zinarejeshwa.

Kipekee kabisa tunamshuku Rais wetu, Mh. Samia Suluhu Hasan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kukatisha safari yake ya kikazi katika Mkutano wa Kilele wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28), huko Dubai na kuamua kurejea nyumbani ili kuwafariji wahanga wa janga hili.

Sisi kama kanisa tunaendelea kuwaombea wafiwa na wahanga wote wapate faraja na ustahimilivu wa haraka na kuwa na subira; na tunashiriki ipasavyo, kupitia taasisi zetu husika, kuleta faraja na kuwahudumia ndugu zetu wa Hanang kwa njia mbali mbali za kiroho na za mahitaji ya kibinadamu.

*"Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote." 2 Wakorintho 1:3*

Mungu Anatawala.

TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD
HEAD OFFICE
P.O. BOX 1760
DODOMA

**Rev. Dr. Barnabas W. Mtokambali**
**Askofu Mkuu, Tanzania Assemblies of God (TAG)**

# TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD

